JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu ya mdomo: (028) 2220215-18
E-mail: ras.kagera@tamisemi.go.tz
Fax: (028) 2222341 / 2221356

OFISI YA MKUU WA MKOA
S. L. P. 299,
BUKOBA - KAGERA.
TANZANIA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
TAREHE 13 APRILI, 2017

Ndugu Waandishi wa Habari, Nimewaiteni hapa ili kutoa taarifa juu ya Operesheni ya kuondoa mifugo na Wananchi wavamizi waliokuwa wakiendesha shughuli za kibinadamu katika Mapori ya Akiba, Hifadhi za Misitu, Mapori Tengefu na Maeneo ya vyanzo vya maji katika Mkoa wa Kagera.

Ikumbukwe kwamba Operesheni hiyo ilianza tarehe 30 Machi, 2017 mara baada ya mimi mwenyewe Mkuu wa Mkoa kutoa amri ya siku tatu kwa wote waliovamia maeneo hayo kuondoka wenyewe kwa hiari kuanzia tarehe 18 hadi 21 Machi, 2017. Aidha, niliamua kuongeza muda huo hadi tarehe 29 Machi, 2017 ili kuwapa muda wa kutosha kuondoa mifugo yao na wao wenyewe kuondoka kwa hiari.

Ndugu Waandishi wa Habari, Amri hiyo niliitoa mara baada ya kufanya ziara mwishoni mwa mwezi Januari 2017 ya kutembelea Misitu ya Hifadhi ya Biharamulo, Nyantakara, Ruiga, na Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi na kujionea hali halisi ya uharibifu wa hifadhi hizo kutokana na shughuli za kibinadamu pamoja na uchungaji wa mifugo katika hifadhi hizo uliokuwa unahatarisha uwepo wa wanyamapori na ustawi wa misitu yetu ya asili.

Ndugu Waandishi wa Habari, ***Utekelezaji:*** Utekelezaji wa Operesheni ulianza tarehe 30 Machi, 2017 katika Misitu ya Hifadhi na Mapori ya Akiba yaliyotajwa hapo juu kwa kuzingatia sheria na bila kumwonea mtu. Opersheni hiyo ilihusisha msako wa ardhini ambao uligawanywa katika Viteule vikuu vitano ambavyo ni Kigombe na Nyanazi (Wilayani Biharamulo), Nyungwe na Sekeseke (Wilayani Ngara) na Bunazi Wilayani Missenyi. Viteule hivyo vikuu vitano viligawanywa katika vituo vidogo vidogo (Sections) 15 ili kurahisisha kazi ya kuyafikia maeneo yote ya hifadhi.

Pia katika Operesheni hiyo vimetumika vifaa vya kisasa kama ndege zenye Rubani na ndege zisizokuwa na Rubani (Drones) ili kuhakikisha kila eneo la Hifadhi linabaki salama bila uvamizi wa mifugo wala shughuli zozote za kibinadamu aidha kuhakikisha lengo kuu la Operesheni hiyo linafanikiwa kwa asilimia 100%.

Ndugu Waandishi wa Habari, ***Mafanikio na Hatua zilizochukuliwa:*** Katika Operesheni hiyo tumefanikiwa kukamata Ng'ombe 5,754 Mbuzi 140, na Kondoo 45, ambapo jumla ya mifugo wote ni 5,939.

Pia watuhumiwa 185 wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria wakiwa na makosa mbalimbali kama; Kuingia ndani ya Mapori ya Akiba na Hifadhi za Misitu bila kibali, Kupatikana na mazao ya misitu na wanyamapori bila kibali, Kulima na kuanzisha makazi ndani ya Hifadhi kinyume cha sheria, Kuchunga mifugo ndani ya Hifadhi za Misitu na Wanyamapori, Kuingia nchini bila kibali na kupatikana na siraha kwenye Mapori ya Akiba.

Ndugu Waandishi wa Habari, Jumla ya kesi 70 za watuhumiwa 130 zimefikishwa Mahakamani katika Mahakama ya Biharamulo ambapo kati hizo, kesi 39 zimemalizika na adhabu kutolewa kwa watuhumiwa waliotiwa hatihani kwa kulipa faini kati ya Shilingi 50,000/= hadi 700,000/= kwa kila kosa ambalo mtuhumiwa ametiwa hatiani. Aidha kifungo cha miezi sita hadi miaka miwili, Kuachiwa huru kwa masharti au kuachiwa huru bila masharti.

Katika Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo kesi 31 zinaendelea kusikilizwa, Mahakama ya Wilaya ya Ngara kesi 16 zilifunguliwa, kesi moja imehukumiwa na kesi 15 zinaendelea kusikilizwa. Aidha, katika Mahakama ya Wilaya ya Missenyi kesi 12 zilifunguliwa ambapo kesi 6 zimehukumiwa na kesi 6 zinaendelea kusikilizwa.

Ndugu Waandishi wa Habari, Katika usimamizi wa kesi za mifugo iliyokamatwa kwenye Hifadhi za wanyamapori, jumla ya mifugo 453 imetaifishwa kwa amri ya Mahakama, na mifugo hiyo inajumuisha ng'ombe 314, mbuzi 122 na kondoo 17.

Aidha, katika utekelezaji wa operesheni mashamba yenye jumla ya ekari 127 ya mazao mbalimbali kama migomba, ufuta, mahindi, karanga, viazi vitamu, mihogo, mtama, maharage, mpunga na bangi katika Hifadhi za Misitu na Wanyamapori yaliteketezwa. Pia vifaa au mali zilizotelekezwa na kukamatwa ni, Magunia ya mkaa 162, Baiskeli 50, Mbao 40, Malori 2, Misumeno 7, Mapanga 7, Pikipiki 7, Mitumbwi 2, Nyavu ya kutega samaki 1, Mitego ya Wire 17, na Mashine za kusaga 3.

Ndugu Waandishi wa Habari, Serikali inasubiri utaratibu wa Kisheria Mahakamani kukamilishwa kwa mifugo iliyotahifishwa na ile itakayoendelea kutaifishwa ili mifugo hiyo iweze kuuzwa kwa njia ya mnada ambapo itauzwa kwa mnada wa wazi na kuruhusu kila mwananchi kushiriki katika mnada huo.

Ndugu Waandishi wa Habari, *Maagizo:* Nawaagiza Wakuu wote wa Wilaya za Mkoa wa Kagera kupitia Kamati zao za Ulinzi na Usalama kuhakikisha wanasimamia kikamilifu maeneo yao ya utawala kupitia viongozi walioko chini yao juu ya mambo muhimu yafuatayo:

Ng'ombe wote waliotolewa ndani ya Hifadhi za Misitu na Wanyamapori na kuegeshwa kando kando ya hifadhi hizo na kupelekea nyakati za usiku kurudishwa hifadhini kuchungiwa huko waondoshwe mara moja katika maeneo hayo yanayopakana na vijiji au makazi ya wananchi.

Pili, *Mwananchi yeyote ambaye amepokea mifugo isiyokuwa yake kwaajili ya kumtunzia mmiliki halali kwa muda achukuliwe hatua za kisheria kwasababu mifugo hiyo itasababisha mfarakanao kati ya Wafugaji na Wakulima ambapo mifugo hiyo huishia kulishwa katika mashamba ya wakulima*.

Agizo la Pili: Nawaagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha wanasimamia kikamilifu **sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya mwaka 2009**, na **Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002.**

Hakikisheni sheria nilizozitaja hapo juu zinasimamiwa kikamilifu ili kulinda hifadhi zetu. Sheria hizo mkizisimamia kikamilifu Mapori yetu ya Akiba na Misitu yetu itakuwa katika hali nzuri. Pia watumishi wa mamlaka tajwa hapo juu nawaasa kutojihusisha na vitendo vya rushwa au uvunjifu wa sheria kwani kwa mtumishi yeyote atakayebainika anajihusisha na vitendo hivyo hatua kali za kisheria zitachukulia mara moja.

Ndugu Waandishi wa Habari, Natoa **wito** kwa wafugaji ambao wameondoa mifugo yao wenyewe ndani ya Hifadhi za Misitu na Wanyamapori kupunguza mifugo yao kwa kufuga kisasa na kuivuna ili kunufaika na mifugo hiyo kuliko kuendelea kufuga na kuzalisha mifugo mingi na kupelekea kukosa malisho na kuvamia hifadhi zetu.

Ndugu Waandishi wa Habari, *Mwisho:* Nawatahadharisha wananchi wote ambao wanadhani kuwa operesheni hii ni ya muda wasithubutu kurudisha mifugo yao katika hifadhi au kuendesha shughuli zozote za kibinadamu katika maeneo hayo kwani operesheni hii ni endelevu na hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja utaifishwaji wa mifugo hiyo moja kwa moja.

Imetolewa na; Mhe. Meja Jenerali (Mst) Salum M. Kijuu,
Mkuu wa Mkoa,
KAGERA.